JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO

17 JUNI, 2016

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO – 17 JUNI, 2016

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu malalamiko yaliyofikishwa kwenye Kamati dhidi ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutuhumiwa kusema uongo na kutoa taarifa ambazo hazina ukweli Bungeni.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

379. MHESHIMIWA FREEMAN AIKAELI MBOWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mfumo wa vyama vingi vya siasa huwapa wananchi fursa ya kuchagua Kiongozi na Chama wanachokitaka sambamba na Ilani za Vyama husika katika kila ngazi ya uchaguzi kuanzia ngazi ya Mtaa/Kijiji, Kata, Jimbo na Taifa:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali ya CCM hupuuza ukweli huu na kulazimisha Ilani ya Chama chao kutekelezwa nchi nzima kila ngazi bila kujali matakwa ya wananchi kupitia uchaguzi;

(b) Je, katika mazingira ya Manispaa au Halmashauri za Wilaya palipo na uongozi wa Chama tofauti na CCM ni ipi mipaka ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa kutoa amri au maelekezo ya kiutendaji;

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuweka utaratibu wa kisheria na kikanuni ili kuondokana na mfumo huu kandamizi ambao ni urithi na ukiritimba wa mfumo wa Chama kimoja cha siasa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

380. MHESHIMIWA ALMASI ATHUMANI MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui yapo Isikizya eneo ambalo halina miundombinu, nyumba za kuishi na huduma rafiki kwa wafanyakazi; Shirika la Nyumba la Taifa limejenga nyumba Isikzya na lilipendekeza kuuza nyumba hizo kwa Halmashauri ya Uyui na kumaliza malipo ndani ya miaka mitatu; lakini Halmashauri haina uwezo wa kumaliza malipo

ndani ya miaka mitatu. Hivyo wafanyakazi wa Halmashauri wanaendelea kuishi katika nyumba za kupanga Mjini Tabora:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchangia ununuzi wa nyumba za Shirika la Nyumba (NHC) ili wafanyakazi wa Halmashauri ya Uyui wahamie Isikizya;

(b) Shirika la Nyumba ni wadau wa maendeleo ya makazi na kwa kuwa Serikali ina nia ya kusaidia uanzishwaji wa Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui; Je, kwa nini Serikali isishawishi Shirika la Nyumba kuongeza muda wa kuuza nyumba zake kutoka miaka mitatu hadi kumi ili kuwezesha Halmashauri kulipa polepole.

381. MHESHIMIWA RASHID MOHAMED CHUACHUA (MASASI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sera ya Serikali ya kujenga Zahanati kwa kila Kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata haijatekelezwa vyema katika Jimbo la Masasi ambapo hakuna Kata yenye Kituo cha Afya cha Serikali na Zahanati zilizopo ni saba tu:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya katika Kata 14 za Jimbo la Masasi;

(b) Je, Serikali inaweza kukiri kuwa kuna haja ya kuzipandisha hadhi Zahanati za Chisegu, Mumbaka na Mwenge Mtapika ili ziwe na Vituo vya Afya na hatimaye kuipunguzia mzigo Hospitali ya Mkomaindo pamoja na kusogeza huduma kwa jamii.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

382. MHESHIMIWA MARGARETH SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Baadhi ya mambo ambayo yanamkosesha mkulima wa Tumbaku mapato stahiki ni pamoja na tozo za pembejeo zinazoingizwa nchini na kuzifanya kuwa ghali, kuwepo wanunuzi wachache wa Tumbaku na hivyo kudumaza ushindani wa bei na uwezo mdogo wa kifedha wa Bodi ya Tumbaku:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuondoa utitiri wa tozo za pembejeo;

(b) Je, hadi sasa Serikali imevutia wanunuzi wangapi kutoka China na kwingineko;

(c) Je, kuanzia msimu wa 2016/2017 Serikali imeiongezea Bodi ya Tumbaku kiasi gani cha fedha katika bajeti yake ili iendeshe masoko ya Tumbaku kwa ufanisi.

383. MHESHIMIWA SAVELINA SILVANUS MWIJAGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Pamoja na Serikali kuwa na mipango mizuri kwa Wananchi wake lakini mipango hiyo baadhi yake haitekelezwi; Wakulima wengi nchini wanalima bila ya kuwa na elimu ya kilimo na hivyo kushindwa kulima baadhi ya mazao ya biashara na ya chakula kama vile Ndizi, Kahawa, Mahindi, Maharage, Karanga n.k:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje Wakulima hao ili wanufaike na kilimo pamoja na mazao yao kwa chakula na biashara;

(b) Je, Serikali ina mipango gani juu ya utoaji wa elimu kwa Wakulima ili wafaidike na kilimo chao.

384. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Sekta ya uvuvi hapa Tanzania inaajiri Wananchi wengi lakini wavuvi hawanufaiki kutokana na changamoto mbalimbali:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia mlundikano wa leseni kwani kuna aina nyingi sana za leseni kwa mfano leseni ya chombo, leseni ya mvuvi, leseni ya aina ya samaki, leseni ya eneo la uvuvi n.k;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi nyenzo za uvuvi ili waondokane na uvuvi haramu;

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

385. MHESHIMIWA ZUBEDA HASSAN SAKURU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na ongezeko kubwa la matukio ya kihalifu nchini yanayohusishwa pia na upatikanaji wa hati za kusafiria zaidi ya moja zinazotolewa hapa Tanzania kwa baadhi ya wahalifu kiholela:-

Je, Serikali inachukua hatua gani katika udhibiti wa utoaji hati za kusafiria kiholela.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

386. MHESHIMIWA DKT. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mradi wa REA II ulitarajiwa kuvipatia umeme Vijiji vyote vya Jimbo la Busega; na kumekuwepo na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huo Jimboni humo:-

(a) Je, mpaka sasa ni Vijiji vingapi vimepatiwa umeme kupitia mradi huo;

(b) Je, ni lini Vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme.

387. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni aina gani ya madini yanapatikana ndani ya Wilaya ya Kalambo kulingana na tafiti ambazo zimekwishafanywa na Serikali.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

388. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Benki ya Wanawake ni chombo muhimu sana hasa kwa wanawake wa Tanzania:-

(a) Je, ni lini litaanzishwa Tawi la Benki ya Wanawake katika Mkoa wa Morogoro ili wanawake wa Morogoro wapate kunufaika na Benki yao;

(b) Je, kuna mkakati gani wa kuanzisha matawi ya Benki ya Wanawake katika Mikoa yote ya Tanzania ili wanawake waweze kukopa kwa urahisi.

III. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE.

DODOMA
17 JUNI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE